

Bibilia ya watoto Inaleta



Mbinguni,
nyumbani
pazuri kwa
mungu



Kimeandikwa na: Edward Hughes

Kimeorodheshwa na: Lazarus;
Alastair Paterson

Imerekebishwa na: Sarah S.

Kimetafsiriwa na: Grace Chepkoech


Kimedhibitishwa na: Bible for Children
www.M1914.org

©2020 Bible for Children, Inc.

License: Kuna ruhusa ya kuchapa hadithi
hii, lakini bila ya kuuza.




Yesu alipokuwa akiishi duniani
aliwaeleza wanafunzi wake
kuhusu mbinguni.



Alipaita "Nyumbani mwa Baba Yangu", na akasema kuwa kule kuna makao mengi ya kupendeza.

Mbinguni ni kubwa na kupendeza




kuliko nyumba yoyote hapa duniani.




Yesu akasema, "Ninaenda
kuwaandalia mahali. Basi mimi
nikienda kuwaandalia mahali, nitakuja
tena niwakaribishe
kwangu."




Yesu alienda mbinguni baada ya
kufufuka kifoni. Wanafunzi wake
wakitazama, Yesu alichukuliwa juu, na
wingu likamchukua ili
wasimwone
tena.



Tangu hapo, wakristo hukumbuka
ahadi ya Yesu kuwa atarudi
kuwachukua. Yesu alisema
kuwa atarudi ghafila,
wakati ambao
hawamtarajii.



Lakini, je wakristo watakaokufa
kabla hajaja? Bibilia inasema
wataenda moja kwa moja
kuwa na Yesu.
Kutokuwa kwa
mwili ni kuwa
na Yesu.




Ufunuo, kitabu cha mwisho cha
bibilia, inatueleza jinsi mbinguni ni ya
ajabu. Kitu cha kushangaza ni kuwa,
katika njia ya kipekee, mbinguni ni
nyumbani mwa Mungu.

Mungu yupo kila
mahali lakini
enzini kwake
ni mbinguni.



Malaika na viumbe
vingine mbinguni
wanamwuabudu
Mungu mbinguni.




Pia watu wote wa Mungu waliokufa
na kuenda mbinguni
wanamwuabudu.
Wanaimba ...




... nyimbo za sifa
kwa Mungu. Haya ni
maneno kutoka wimbo
moja wao huimba:




WEWE UNASTAHILI
KWA KUWA WEWE
UMETUREJESHA ...



... KWA MUNGU
KUPITIA DAMU
YAKO KWA KILA
KABILA NA TAIFA
NA ...




... UMETUTENGENEZA
WAFALME NA
MAKUHANI KWA
MUNGU WETU.
(Ufunuo.
5:9)



Kurasa za mwisho katika bibilia
zinaelezea mbinguni kama
"Yerusalemu Mpya". Ni kubwa
ajabu,

ikiwa
na
kuta
za juu
nje.



Kuta zimeundwa kwa yaspi, mfano wa kioo safi. Vito vya ajabu vimepamba kuta, ziking'aa na rangi za kupendeza.


Kila mlango




imeten-
genezwa
na lulu
moja
kubwa!




Hiyo milango ya lulu huwa wazi kila wakati. Tuingie ndani tukaone zaidi...
WAAA! Mbinguni ni ya kupendeza hata zaidi ndani.




Mji ule ni wa dhahabu safi, kama kioo
kiangavu. Hata njia ni ya dhahabu.




Mto wa maji safi ya uzima, wenye kung'aa unatirirka ukitoka katika kiti cha enzi cha Mungu. Upande huu na upande ule wa mto kuna mti wa uzima, ambao ulipatikana kwanza katika bustani ya Edeni.




Mti huu ulikuwa wa kipekee. Ulikuwa unazaa matunda aina kumi na mbili, wenye kutoa matunda aina tofauti kila mwezi. Na majani ya mti huo ni wa kuponya mataifa.




Mbinguni haiitaji jua wala mwezi
kuangaza. Utukufu wa Mungu hutia
nuru ya ajabu. Hakuna usiku kule
hata kamwe.



Hata wanyama mbinguni ni wa aina tofauti. Wote ni watulivu na wenye urafiki. Mbwa mwitu na mwana kondoo wanakula nyasi pamoja.



Hata simba wanakula nyasi
kama ng'ombe. Bwana anasema,
"Hawataumia wala kuangamia katika
mlima wangu mtakatifu."



Tunapozidi kutazama, tunagundua
kuwa kuna vitu vinavyokosa
mbinguni.

Hakuna
maneno
ya
hasira.

Hakuna
mtu

anayepigana au kunyima.




Hakuna vifunguo mlangoni kwa kuwa
hakuna wezi mbinguni. Hakuna
waongo,
wauaji,
wachawi
au watu
wengine
waovu.
Hakuna
dhambi ya
aina yoyote mbinguni.




Mbinguni kwa Mungu
hakuna kilio tena.
Wakati mwingine watu
wa Mungu hulia
kwasababu ya mateso
makuu ya maisha haya.
Mbinguni, Mungu
atapanguza machozi
yote.




Hakuna kifo mbinguni pia. Watu wa
Mungu watakaa milele na Bwana.
Hakutakuwa na
mateso, kilio,
uchungu
tena.



Hakutakuwa na magonjwa, kuachana,
matanga tena. Kila mtu ataishi kwa
furaha na
mungu.




Kupendeza zaidi, mbinguni ni ya wasichana na wavulana (na watu wazima pia) ambao wamemwamini Yesu Kristo kama mwokozi na kumtii kama Bwana wao.




Mbinguni kuna kitabu kiitwacho
Kitabu cha Mwana kondoo cha
Uzima. Kimejaa majina ya watu.
Je, wajua ni majina ya nani
yaliyo andikwa? Ni
watu ambao
wameweka
tumaini yao
kwa Yesu. Je,
jina lako limo
ndani?



Maneno ya mwisho ya bibilia ina
ukaribisho wa ajabu. "Na Roho na
Bibi-arusi wasema, 'njoo!'"



Naye mwenye kiu aje. Na yeye
atakaye, na ayatwae maji ya
uzima bure."



Mbinguni, nyumbani pazuri kwa mungu

Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu,
Bibilia,

inapatikana katika

Yohana 14, Wakorintho a pili 5,
Ufunuo 4, Ufunuo 21-22

"Kufafanusha maneno yako kwatia nuru."
Zaburi 119:130



Mwisho



Hii hadithi ya bibilia inatueleza kumhusu
Mungu wetu wa ajabu aliyetuumba na
anayetaka tumjue.

Mungu anajua tumetenda mambo mabaya,
anayoyaita dhambi. Adhabu ya dhambi ni
mauti, lakini Mungu anakupenda sana hata
akamtuma mwana wake wa pekee, Yesu, Ili
afe msalabani na aadhibiwe kwa dhambi
yako. Alafu Yesu akafufuka na kuenda
nyumbani mbinguni! Ukimwamini Yesu na
kumwomba msamaha kwa dhambi yako,
Atakusamehe! Yesu atkuja na kuishi ndani
yako, na utaishi naye milele.



Kama unaamini huu ni ukweli, Sema haya
kwa Mungu:

Mpendwa Yesu, ninaamini kuwa wewe ni
Mungu, na ulifanyika mtu ili ufe kwa ajili ya
dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya, na
siku moja nitaenda kuwa nawe millele.
Nisaidie nikutii na niishi kwa ajili yako kama
mtoto wako. Amina.

Soma bibilia na uzungumze na Mungu kila
siku! Yohana 3:16

